OFISI YA RAIS TAMISEMI
HALMASHAURI YA MANISPAA YA TEMEKE
SHULE YA SEKONDARI MIBURANI

S.L.P 45264, DAR ES SALAAM

PMBR/SEC/VOL. **Tarehe ……..**

Kumb Na ……

Mzazi/Mlezi wa……..…….

S.L.P……

DAR ES SALAAM.

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MIBURANI WILAYA YA TEMEKE MKOA WA DAR ES SALAAM MWAKA 2021

1.0 Utangulizi

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha **kwanza** katika shule hii mwaka **2021**. Shule ya Sekondari **Miburani** ipo umbali wa mita 150 kutoka Hospitali ya Wilaya ya Temeke.

Muhula wa kuanza masomo unaanza tarehe **11 – 01 – 2021.** Unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe **04– 01– 2021** na mwisho wa kuripoti ni tarehe **30– 01 – 2021**.

2.0 Mambo muhimu ya kuzingatia

2.1 Sare za Shule.

(a) SARE/ VAZI RASMI LA SHULE (WAVULANA)

(i) Suruali mbili (2) kitambaa cha Dark Brown

(ii) Shati nyeupe mbili (2) (Tetron) mikono mifupi

(iii) Viatu vya ngozi vyeusi (jozi 2)

(iv) Soksi nyeusi (jozi 2)

(v) Begi la ngozi nyeusi la kubebea vitabu

(vi) Nembo ya Shule (Emblem) mbili (2)

(vii) Tai moja

(b) SARE/ VAZI RASMI LA SHULE (WASICHANA)

(i) Sketi mbili (2) za Dark Brown

(ii) Shati mbili (2) nyeupe (Tetron) mikono mifupi

(iii) Viatu vya ngozi vyeusi (jozi mbili). Visiwe na visigino virefu, visiwe vinapiga kelele na visiwe vya wazi

(iv) Soksi nyeupe ndefu (stocking) zisizo za kuonesha mwili

(v) Begi la ngozi nyeusi la kubebea vitabu

(vi) Nembo ya shule (Emblem) mbili (2)

(vii) Hijabu seti 2 nyeupe (kwa waislamu wanaopenda).

2.2 Vifaa vya mwanafunzi darasani

Madaftari 10, kalamu ya wino (pen) nyeusi au bluu, kalamu ya risasi (pencil) na mkebe wa hesabu (mathematical set Instructions)

3.0 Sheria na kanuni muhimu za shule hii.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

(a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.

(b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.

(c) Kuwahi katika shughuli za shule na nyingine utakazopewa.

(d) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.

(e) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.

(f) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.

(g) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote; na

(h) Kutunza mali za umma.

3.2 Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa shule.

(a) Wizi

(b) Uasherati na ushoga

(c) Ubakaji

(d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika.

(e) Kupigana au kupiga

(f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma

(g) Kudharau Bendera ya Taifa

(h) Kuwa mjamzito au kupata mimba

(i) Kuoa au kuolewa

(j) Kutoa mimba

(k) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.

(l) Kukataa adhabu kwa makusudi

(m) Kuwa na simu mkononi.

4.0 Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na mwanafunzi.

(a) "Medical Examination Form" ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule mara utakapiripoti shuleni.

(b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.

(c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

(d) Tafadhali, soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII.

……..……

MKUU WA SHULE

KIAMBATISHO A

TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI NA MZAZI/MLEZI

A: TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI

1) Jina kamili la Mwanafunzi……
2) Tarehe ya kuzaliwa…….
3) Taifa ……
4) Uraia……
5) Dini …….
6) Shule ya msingi……..
7) Tarehe ya kutoka shule hiyo…….

PICHA YA MWANAFUNZI

B: TAARIFA BINAFSI YA MZAZI/MLEZI

1) Jina kamili la Mzazi/Mlezi…….
2) Kama ni mlezi, uhusiano …….
3) Anuani kamili mjini……
4) Sehemu unayoishi…….
5) Mtaa ……
6) Nambari ya Nyumba……..
7) Nambari ya simu……

PICHA YA MZAZI/MLEZI

C: MAELEZO YA KIKAZI YA MZAZI/MLEZI

1) Jina la Mwajiri na idara……..
2) Anuani yake……
3) Namba ya simu……
4) Kazi ya Mzazi (Meneja, Karani, Daktari, Mfanya biashara n,k)……

D: SOMO LA DINI

Mimi……..ambaye ni Mzazi/Mlezi wa mwanafunzi…….kidato cha ……....
ninaruhusu mtoto wangu kuhudhuria somo la dini ya ……
dhehebu la …….siku ya jumatano akiwa shuleni Miburani Sekondari.

Sahihi ya Mzazi/Mlezi……..

KIAMBATISHO B

FOMU YA KIAPO/AHADI

KWA MWANAFUNZI

Mimi …… ……..(jina kamili) ninakubali nafasi niliyopewa kuingia kidato cha …… mwaka……. Katika shule ya Sekondari Miburani, Ninaahidi kwamba.

1) Nitatii sheria zote za shule kama nilivyozisoma
2) Nifanya bidii katika masomo, kazi na shughuli zote za shule
3) Nitashiriki kikamilifu katika shughuli za usalishaji mali, kuzalisha mali iliyobora bila kuitia hasara shule kwa kuharibu au kupoteza malighafi ya kuzalishia mali
4) Nitakuwa mwanafunzi mwenye nidhamu ya hali ya juu mkakamavu na mwenye mwenendo safi wakati wowote hata nikiwa nje ya shule kwa madhumuni ya kuipa na kutunza sifa ya Shule ya Miburani Sekondari.

MUNGU NISAIDIE !!!!!!
SAHIHI YA MWANAFUNZI……..

KWA MZAZI/MLEZI

Mimi (jina kamili la Mzazi/mlezi) ……
Mzazi/Mlezi wa ……

Naahidi kwamba:-

1) Nitampatia mwanangu mahitaji ya shule kama yalivyotajwa katika maelekezo ya kujiunga na shule.
2) Nitakuwa tayari kutoa msaada wowote utakaohitajika (Maoni, adhabu) katika kumlea mwanangu
3) Nitamhimiza mwanangu kufanya mazoezi ya masomo yake nyumbani (Home work) na kufuatilia maendeleo yake na tabia yake shuleni.
4) Mwanangu akiwa nyumbani nitamtunza na kumwangalia vizuri mwenendo wake

SAHIHI YA MZAZI/MLEZI……

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

STATION:……

DATE:……

PART A:
TO

Medical Officer.
……
……

Miss/Mr ……...

Please examine the above named as his/her fitness for admission as a student in the following common diseases/problems.

Put (√) for positive and a cross (X) for negative against in a box provided

Pregnancy	
Sight	
Diabetes	
Worms (stool)	
Epilepsy	
TB(Tuberculosis)	
Sickle Cell	
Heart Disease	
Yellow Fever	
U.T.I	
Hearing	
Asthma	

PART B: MEDICAL CERTIFICATE
(To be completed by a Medical Officer)

I have examined the above named and consider that she/he is physically FIT/UNFIT for admission as above.

Date….……Signature……

Station…….……..Designation……